TANGAZO LA SERIKALI Na. 743 La Tarehe 9/12/2022

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI,
(SURA YA 414)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha17)*

AMRI YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MBULU (MBULU WSSA) YA MWAKA 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira za Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbulu (Mbulu WSSA) ya Mwaka 2022.

Marekebisho ya bei

2. Bei za maji safi na usafi wa mazingira za Mbulu WSSA zinarekebishwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Amri hii.

Masharti

3.-(1) Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) miezi mitatu baada ya kuanza kutumia bei na ada zilizoainishwa kwenye Amri hii, Mbulu WSSA itapaswa kupeleka ushahidi kwa EWURA kwamba iliwataarifu wateja wake kuhusu Amri mpya ya bei na kwamba iliwafahamisha ipasavyo wadau wake ikiwa ni pamoja na viongozi wa Serikali, viongozi wa kisiasa, viongozi wa dini, wateja wake, miongoni mwa wengi wengine, juu ya mabadiliko ya bei;

(b) ifikapo tarehe 31 Disemba 2022 au kabla, Mbulu WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa

kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(c) Mbulu WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(d) Mbulu WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(e) Mbulu WSSA itahakikisha kuwa wateja wote wasio na dira za maji wanafungiwa dira za maji ifikapo tarehe 30 Juni 2023;

(f) Mbulu WSSA itaandaa na kutekeleza mpango wa kuwafikia wateja wote na kuwasilisha kwa EWURA taarifa ya utekelezaji wa mpano huo kila mwaka;

(g) Mbulu WSSA itahakikisha hesabu zake za fedha zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuwasilisha taarifa ya ukaguzi kila mwaka; na

(h) Mbulu WSSA itashirikiana na Halmashauri ya Mji wa Mbulu ili kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka ifikapo tarehe 30 Juni 2023.

(2) Mbulu WSSA itapaswa, kila mwaka na kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri hii.

(3) Mbulu WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA na EWURA itazitumia taarifa hizo katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mbulu WSSA ikilinganishwa na mamlaka nyingine za majisafi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake.

Kufutwa kwa Amri Na. 11-014 ya 2011

4. Amri Na. 11-014 ya tarehe 1 Juni 2011 ya eneo la huduma la Mbulu WSSA inafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa

| Kundi la Wateja | Kipimo | Bei za Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | Sh./Mita ya ujazo | 540 | 1,210 | 1,420 | 1,440 |
| Taasisi | | 550 | 1,430 | 1,460 | 1,480 |
| Biashara | | 560 | 1,490 | 1,500 | 1,510 |
| Viwanda | | 570 | 1,500 | 1,510 | 1,530 |
| Magati | Sh./Lita 20 | 10.0 | 20.0 | 25.0 | 25.0 |
| WASTANI | Sh./Mita ya ujazo | 542 | 1,266 | 1,428 | 1,447 |

Jedwali Namba 1(b): Bei za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi kwa Mwezi)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa |
|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 |
| Majumbani | 4,500 | 13,000 |
| Taasisi | 10,000 | Hairuhusiwi |
| Biashara | 9,500 | Hairuhusiwi |

Jedwali Namba 1(c): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 150,000 | 26,000 | | |
| Taasisi | 170,000 | 26,000 | | |
| Biashara | 170,000 | 26,000 | | |
| Viwanda | 170,000 | 26,000 | | |

Jedwali Namba 1(d): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji (Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Taasisi | 11,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 11,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | - | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya 3(1)(c))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| Na. | Maelezo | Gharama (TZS) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| 1 | Kukarabati miundombinu ya maji na mabomba ya mradi wa maji wa Daudi | | 11,000,000 | |
| 2 | Kukarabati miundombinu ya maji na mabomba ya miradi ya maji ya Bargish na Silaloda | | | 11,000,000 |
| 3 | Ujenzi wa uzio kuzunguka vituo vya kusukuma maji kama ifuatavyo: | | | |
| 3.1 | Kujenga uzio kuzunguka kituo cha kusukuma maji cha kisima cha Ayamohe | | 5,000,000 | |
| 3.2 | Kujenga uzio kuzunguka kituo cha kusukuma maji cha kisima cha Endagikoti | | | 5,000,000 |
| 4 | Kukarabati jengo la kituo cha kusukuma maji cha Endagikoti | | | 25,000,000 |
| 5 | Kukarabati miundombinu ya mfumo wa umeme kwenye kituo cha kusukuma maji cha Endagikoti | | 6,000,000 | |
| 6 | Kukarabati kuta na sakafu ya juu ya tanki la Magereza lenye ujazo wa $90m^3$ | | 15,000,000 | |
| 7 | Kukarabati kuta na sakafu ya juu ya tangi la Hayahaya lenye ukubwa wa mita za ujazo 135 | | | 20,000,000 |
| 8 | Kujenga uzio kwenye maeneo ya matangi manne yaani Ayamaami, Tango, Khaday na Ayamohe | | 7,000,000 | 21,000,000 |
| 9 | Kukarabati tangi la Tango FDC lenye ujazo ukubwa wa | | 25,000,000 | |

*Tangazo la Serikali Na. 743 (Linaendelea.)*

| Na. | Maelezo | Gharama (TZS) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| | mita za ujazo 135 | | | |
| 10 | Kubadilisha mtandao wa mabomba wenye urefu wa kilomita 4.5 katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo | | | |
| 10.1 | Kujenga upya km 0.5 za bomba | 7,500,000 | | |
| 10.2 | Kujenga upya km 1 za bomba | | 15,000,000 | |
| 10.3 | Kujenga upya km 3 za bomba | | | 32,000,000 |
| 11 | Ununuzi wa Dira za Maji kama ifuatavyo: | | | |
| 11.1 | Kununua dira mpya 600 na vifaa vyake | 60,000,000 | | |
| 11.2 | Kununua dira mpya 1575 na vifaa vyake | | 157,500,000 | |
| 11.3 | Kununua dira mpya 1575 na vifaa vyake | | | 160,000,000 |
| 12 | Kununua na kufunga dira maji 288 kwa kwa wateja wasio na dira | 28,800,000 | | |
| 13 | Kununua na kubadilisha dira za maji kama ifuatavyo | | | |
| 13.1 | Kununua dira mpya 550 kwa ajili ya kubadili dira za zamani na zilizoharibika | | 57,200,000 | |
| 13.2 | Kununua dira mpya 600 kwa ajili ya kubadili dira za zamani na zilizoharibika | | | 64,200,000 |
| 13.3 | Kununua na kufunga dira za malipo ya kabla 50 | | | 26,250,000 |
| 14 | Kununua dira kubwa mbili (2) kwa ajili ya vyanzo vya maji vya Enderer Indirim na Endagikot | 7,000,000 | | |
| 15 | Kununua dira kubwa 17 kwa ajili ya vyanzo vya maji vya Ayamohe na Endagikoti na matoleo ya matangi(8 kwa mwaka 2023/24 na 9 kwa mwaka 2024/25) | | 24,000,000 | 27,000,000 |
| 16 | Kununua na kufunga valvu 65 (sluice valves), 5 kwa mwaka 2022/23, 10 kwa mwaka 2023/24 na 50 kwa mwaka 2024/25 | 6,000,000 | 12,000,000 | 60,000,000 |
| 17 | Kujenga chemba 46 kwa ajili ya valvu zilizopo ( 20 kwa mwaka 2023/24 na 26 | | 10,000,000 | 13,000,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 743 (Linaendelea.)*

| Na. | Maelezo | Gharama (TZS) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| | kwa mwaka 2024/25 | | | |
| 18 | Kununua vitendea kazi ikiwa ni pamoja na viungio na spana | 5,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 |
| 19 | Kununua viti 11 na meza 4 | | 5,300,000 | |
| 20 | Kununua viti 12 vya ofisi, meza 4 na kabati moja | | | 7,100,000 |
| 21 | Kununua kompyuta mbili kwa ajili ya shughuli za ankara na utawala | 3,000,000 | 3,000,000 | |
| 22 | Kununua printa moja yenye kinukuzi (photocopier) | | 7,000,000 | |
| 23 | Kununua kompyuta mbili na printa moja | 5,000,000 | 3,000,000 | |
| 24 | Kununua pikipiki mpya nne kwa ajili ya shughuli za mauzo | 4,800,000 | 4,968,000 | 5,141,880 |
| 25 | Kununua pikipiki 2 kwa ajili ya shughuli za kiufundi | | 9,600,000 | |
| | Jumla ya Gharama | 127,100,000 | 391,568,000 | 490,691,880 |

---

JEDWALI LA TATU

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(1)(d))*

---

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Maelezo | Kizio | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Maunganisho Mapya ya Majisafi | No. | 500 | 800 | 1,000 |
| Upotevu wa Maji | % | 35 | 30 | 28 |
| Kiwango cha Kufunga Dira za Maji kwa Wateja | % | 100 | 100 | 100 |
| Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato | % | 95 | 95 | 95 |

Dodoma
28 Novemba, 2022

MODESTUS M. LUMATO,
*Mkurugenzi Mkuu*